

Mradi wa Isak na Allison



Huyo ni Lulu

Lester. Yeye ni Mmarekani. Alizaliwa Bloomington Indiana. Bloomington iko kati ya Indianapolis na Louisville. Blomington ni mji mdogo kuliko Babati lakini Bloomington ni mji mkubwa kuliko Bagamoyo. (Babati na Bagamoyo ni miji nchini Tanzania.) Bloomington ina takriban watu elfu sitini na tisa, mia mbili na ishirini na nane. Bloomington ina maduka na ina mikahawa mingi kama "McDonalds," "Burger King" na "Steak and Shake." Lakini Lulu hakulelewa Bloomington. Kwa kweli, alilelewa wakati wa matatizo. Kila mmoja, Mama na Baba yake walienda Tanzania kutembelea marafiki zao wakat Lulu alipokuwa mtoto mdogo, lakini wao walipotea!



Kwa hivyo, Lulu alikaa mwituni na wanyama walimlea. Alisahau familia yake na sasa anaweza kusema lugha ya wanyama.

Kila mmoja, wanyama walimwambia Lulu kuhusu familia yao na. Walisema: "Lulu, wewe huwezi kukaa hapa... unahitaji kuenda kutafuta familia yako Tanzania!". Kwa hivyo, Lulu aliondoka kutoka mwituni na alienda kituo cha ndege.



Wakati alipowasili kituo cha ndege mpokezi mmoja alimwambia kuwa atahitaji tiketi kuweza kuenda Tanzania. Lakini Lulu hakuwa na pesa kwa sababu wakati alipokaa ndani ya mwituni yeye hakuwa na kazi. Kwa hivyo alihitaji kutafuta kazi ili aweze kupata pesa.

Alianza kufanya kazi Wall Mart. Alifanya kazi huko kwa miezi mitatu lakini hakupata pesa za kutosha. Kwa hio alienda serikali kuomba pesa, lakini mfanyakazi wa serikali alimwambia "hatuna pesa sasa.... hata hivyo, uwezo wa kiuchumi wa serikali

hauwezeshi kutoa mikopo" lakini Lulu akasema "sipendi mikopo!... ninapenda pesa bure." Mfanyakazi wa serikali alicheka sana.

Siku moja Lulu alijaribu bahati nasibu. Alinunua tiketi. Lulu alingojea siku kuwasili. Hakufikiri atashinda bahati nasibu. Wakati ulipokuja, Lulu alikuwa na wasi wasi ya matokeo. Hakukaa kitako. Alikuwa na wasi wasi! Alijaribu kulala, lakini Lulu Lester hakuweza kulala. Alijaribu kula, lakini hakuweza kula. Alijaribu kuangalia sinema, lakini hakuweza kuangalia. Hatimaye matokeo yalitokea. Alishinda! Lulu Lester alishinda! Alifurahi sana!! Alishinda dola milioni mbili! Lulu ni mtu aliyefurahi. Yeye alimpigia simu Simba.

Lulu Lester anampenda Simba sana na Simba ni rafiki wa Lulu Lester bora zaidi. Simba ni mzuri sana. Simba alipenda kusaidia watu. Pia alipenda wanyama. Aliwasaidia wanyama na watu siku kutwa. Simba alisoma siasa na sheria. Alitaka kubadili dunia.

Lulu Lester alimpigia simu Simba. Simba alisema kwenye simu, "Hujambo?" Lulu Lester alijibu, "Sijambo!" Simba alijibu, "AHH!! Lulu!! Habari gani?" Lulu alijibu, "Nzuri sana!!!! Nimeshinda bahati nasibu!! Nimeshinda dola milioni mbili!!" Simba alijibu, "Lulu!!! Hilo ni jambo la ajabu!!!!" Lulu alijibu, "Asante! Ninataka kukualika uje na mimi Tanzania. Tutasafiri Tanzania. Ninataka kuwatafuta mama yangu na baba yangu." Simba alijibu, "ASANTE!! NDIO, NDIO!! Tutawatafuta mama yako na baba yako." Lulu alijibu, "Nimefurahi sana." Simba alijibu, "Tarehe gani?" Lulu, "Ninafikiri tuondoke kesho." Simba alijibu, "Ndio!!" Lulu alijibu, "Nitapata tiketi. Nitanunua tiketi. Tutaonana!" Simba alijibu, "Tutaonana, Lulu!!" Simba alisisimuka! Lulu alinunua tiketi mbili. Simba na Lulu walikuwa hawana mipango ya wakati wa kiangazi. Lulu na Simba walisimuka.